Tuheshimu ofisi wa Rais na tuheshimu kiti cha Rais kwa sababu tuko hapa kama sisi ni watoto wake na tuko kukaa kwa amani na umoja. Tuheshimu kabisa na kumombea hekina na tunamoumbea Mungu apate nguvu ya kuongoza nchi. Hakuna njia ingine kwa sababu ananichunga mimi na watoto wangu nakila mtu.

**Com. Riunga Raiji:** Nafikiri hiyo tumesikia na hiyo ilikuwa ya mwisho lakini kwa sababu wewe ni mzee nimekuongeze saa ingine kidogo. Okay asante sana mzee.

**John Mutai:** Wacha niseme moja. Kuna jambo moja ambayo mimi naona katika hii Kenya yetu na ni baya kidogo. Saa zingine unasikia kumeuwawa ma- Padri mwingine bila hatia hiyo inatakiwa ikomeshwe kwa sababu hao ni watu wa Mungu. Halafu mnasikia wameuwawa nama hii.

Nikimalizia, sina mengi nikuiongea juu ha hiyo haki yetu. Tuandike Katiba yetu ile ambayo inatujenga sisi na iel ambayo sisi tukaa.

**Com. Riunga Raiji:** Sasa mzee hiyo ingine tutaongea tukitoka kwa sababu saa yako imezidi kabisa.

**Joel Mutai:** Tukiwa hapa kuna neno moja ambao nauliza kwa ----, mtu kama yuko na yeye ni Mnandi mimi isiwezi labda---- mtu akiona mambo ya clashes inatokea nini na nini inatokea mtu anaweza kujitokeza na kusema hiyo ni mfano. Mimi sisemi Wanandi ni wajinga, mtu anasema “unaona hao Wanandi wajinga” na watu ikiwafikia namna hiyo ndio mambo yanatokea onaona watu wanaumizana ni mambo kama hayo. Asante sana.

**Com. Riunga Raiji:** Sasa ni Julius K. Tot. Jiandikishe hapo. Julius K. Tot, hayuko? Mirriam Kogo, hakuna. John Metto ni wewe? Utafuatwa na Kiptunge Sitenei. Kama kuna ingine tupatie Memorandum tutasoma jiandikishe ili tumpatie nafasi Kiptunge Sitenei, Bwana Sitenei yuko? Councillor David Rotich.

**Clr. David Rotich:** Mimi kwa majina naitwa David Cheruiyot Rotich ni mkaaji wa Inamotui location. Maoni ni kana ifuatavyo. Kulingana na marekebisho ya Katiba ya nchi ambayo tunafanya sasa, ningenelea sheria ya nchi hii ituzwe sana. Ukiangalia sheria ya Kenya ambayo tulikuwa nayo karibu three quarter ilikuwa nzuri lakini ubaya haikutuzwa. Ukiangalia sheria kama ya nchi ya Uganda wanaituzwa sheria sawa kabisa lakini Kenya walirengesha uwezo wa kutuza sheria sawa. Kwa hivyo tunaomba sheria ituzwe kabisa katika Kenya hii.

Ningependeza vyama vya kisiasa ziwepo na visizidi kumi na visiwe vya kikabila.

Tuwe na mfumo wa Majimbo ambao rasilimali zake ama uwezo utakuwa katika provincial na mali ama rasilimali ya sehemu hiyo itakuwa katika county council.

Tuwe na mzee wa mtaa ambaye atapewa mshahara. Tuwe na Assistant chief na Chief na ambao wananchi wenyewe wamewachagua. Tuwe na DO, DC na PC ambao watapewa appointment na Parliament. Tuwe na Prime Minister na President na President awe ceremonial President.

Mali ana ukusanyaji wa mali ya nchi: Iwapo itafanywa na central government ama jimbo na utasimamiwa na Nandi county council ata kama mali imetoka ng'ambo lakini itaenda direct kwa Nandi county council. Inayofuata ni mambo ya rasilimali kama maji, msitu, ---na madini yote yaende katika Nandi county council na more than 30% irudi kwa mwananchi mwenyewe.

Sheria ya kulinda viwanda: Ukiangalia Kenya yetu viwanda vyetu vimeharibiwa na mambo ya corruption kwa hivyo tunaitaji sheria ambayo inalinda viwanda katika nchi yetu ya Kenya. Nilikuwa nimesema uongozi wa Majimbo ili uongozi uweze kutoka katika sehemu bali bali usiwe umetoka sehemu moja headquarter kama Naiorbi peke yake.

**Com. Riunga Raiji:** Dakika moja.

**Cllr. David Rotich:** Mbona umekata yangu sana? Tea estates katika Nandi iwe under Nandi county council. Public utility ziwe zimetuzwa, zituzwe kabisa.

Freedom of worship – uhuru wa kuabudu: Katika Kenya tunapata siku ya kuabudu ni Friday, Saturday na Sunday, watu wapate uhuru wa kuabudu na iwe ni Mungu peke ambaye anaabudiwa.

Katika nchi hii tumepoteza watu wengi kwa sababu ya Ukimwi. Mapendekezo yangu mtu ambaye ako na AIDS ajulikane kama nchi zingine. Pengine inaweza kuwa inanihusu ninaomba katika Kenya hii watu wote wanapewa na wanalipwa mshahara. Na Councillors wa Kenya hii wanapewa kitu kana sitting allowances kwa hivyo ningepomba wapewe mshahara na benefits zingine kama wengine Kenya hii. Nchi zingine ukiangalia serikali inasimamia kitu cha kuuzwa kwa hivyo ningependelea wananchi waweze kufanya kazi, kupanda mimea na serikali iweze kutafuta mahali pa kuuza.

**Com. Riunga Raiji:** you are on your last point it is already five minutes.

**Cllr. David Rotich:** Two only please. Ninafaa tuwe na Constitutional Commissioners kama Human Rights, Gender Commission, Anti-corruption Commission na Elders Commission.

Ni jukumu la serikali kuwapatia watu wake kazi, usalama, afya, maji, masomo na vyakula. Inafaa kila mtu awe na shamba isiozidi acre mia moja. Asante.

**Com. Riunga Raiji:** Okay Bwana Councillor asante sana. Tafadhali tupatie Memorandum. Samuel Kibenei, hayuko. Bwana Kiplagat Biwott, hayuko? Huyu mwingine nafikiri ni Kajiro. Utatuambia majina yenyewe. Okay karibu.

**Kajiro Chepkwony:** Mimi ni Kajiro Chepkwony, Ogiek community. Mimi ni chairman ambaye anaongoza Ogiek. Katika Kenya kwa yale makabila arubaini na mbili ambao hawako ndani –

**Com. Riunga Raiji:** Ngoja mzee, namuomba ata nyinyi wanafunzi tafashali mtenge masikio tu msikilize, wacheni watu wazungumze na kuheshimu matamshi ya kila mtu. Endeele mzee.

**Kajiro Chepkwony:** Basi ninaomba Constitution of Kenya Review Commission katika hii kabila kuna aina bila ambazo ziko Kenya ambazo haziko. Na Ogiek tuomba tuwe kabila rubaini na tatu pamoja na Ogiek. Sisi tunaomba kwa sababu Ogiek in watu wachache katika Kalenjin lakini kwa wakati huu sio wachache sana na tunaomba Ogiek wapawe district yao halafu hata sisi tupate Bunge na viongozi wengine. Makao wa Ogiok kwa upande wa Kericho, Mau forest, ole ruone Tilet, Molo, Elbarlgon, Tinderet, -----Kipkerere, Rorengi, Kimsongi, Kalterwa, Saget, -----londiani forest training centre. Kwa hivyo tunaomba Constitution isimamie Ogiek ata sisi tuwe katika kabila arobaini na tatu katika Kenya. Kulingana na uongozi



wa Kenya ama kufutana na uongozi wa Kenya mwito ambao unaongoza nchi hii unaongoza kulingana na yule mtu amepata kura nyingi kama ni mzee ama kijana ama mama anaweza kuongoza nchi hii kwa ajili ya kura nyingi.

Nchi ya Kenya ninaomba wawe wakiongoza Kenya hii watu watatu. Rais, Waziri, Governor na wale viongozi wengine ambao wanakuweko kwa ajili yake. Kulingana na hapa Nandi tuko na mto mmoja msituni ambao unaitwa Cheplang. Hiyo maji kuna wazungu ambao wanakuja hapa na kufunga hiyo maji na kuwakisha stima lakini hao wenyewe hawapatii wale wananchi ambao wanaishi karibu na hiyo mto. Na tunaomba watupatie hata sisi stima. Vile vile wakati wanafungua huo mto kuna maji imechafuka sana hata ng'ombe yenyewe haikunywi na tunaomba hawa wapatie wananchi maji safi ikiwa kuna wakati ambao wanasafisha hiyo mifereji yao wananchi hawawezi kutimia hayo maji.

Vile vile kulingana na wale watatu ambao nilisema wataongoza nchi hii na kutakuwa na serikali ya Majimbo. Inaonekana Majimbo wakati wazungu walikuwa nchi hii zamani tulikuwa na serikali ya Majimbo kwa sababu kila kabila ilikuwa haiwezi kuingia katika makao ya wengine. Lakini wakati tulipopata uhuru kuna amri ingine ilisemekana kuwa kila mtu anaweza kuenda pahali popote katika Kenya na je ninauliza nikiwa hapa Nandi, ama sehemu yoyote, ama rift valley wale Wakalenjin ambao wanaishi Rift valley kama hawezi kuingia district zingine za makabila wengine? Lakini ninaomba Constitution eheshimu district ya kila kabila.

**Com. Riunga Raiji:** Mzee sena point ya mwisho.

**Kajiro Chepkwony:** La mwisho. Kuna watoto ambao wanalemewa wale ambao hawajiwezi na ata mtu mkubwa anaweza kutojiweza. Nitaka wale watu walemavu wasaidiwe na serikali kusomesha watoto wao na kutibiwa katika hospitali.

**Com. Riunga Raiji:** Hiyo ndiyo intakuwa ya mwischo kabisa.

**Kajiro Chepkwony:** Inaweza kuwa bahati baya au nzuri mwanamke anazaa watoto wawili ana watatu na kama mwanamke amesha zaa watoto wawili au watatu hawa wanafaa kutuzwa na serikali. kwa hivyo ninaomba serikali iwaheshimu.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana, jilandikishe hapo mzee. Na mwingine atakuwa ni Joel Keino. Kama hayuko John Murei – hayuko. Samuel Singilai Misoi, karibu mzee utafutwa na Moses Churuoni.

**Samuel Sigilai Misoi:** Yangu ni mafupi sana. Mara kwa mara tunasikia tangu asubuhi umesikia watu amboa wanaitwa Wakalenjin. Naitwa Samuel Sigilai Misoi. Nafiiria mshakaa kwa muda mrefu unasikias hawa Wakalenjin wakililia hizi mipaka wao. Kwa hivyo mimi ni mmoja wao wakuongeza juu ya hizi mipaka iheshimiwe kama vile Mwenyezi Mungu alivyo iweka mbeleni. Kama unavyo sikia kamaba sehemu za Moroni, sehemu ----- serikali inataka kupea watu wengine eheshimiwe na irudishwe pahali ilikuwa mbeleni. Mtu akitka kuishi ndani na Nandi lakini mapaka iwe pale pale. isisongeshwe maanake

tunaweza kumukosea Mwenyezi Mungu. Ata mara kwa mara mnapoona watu wanagongana gongana kwa ajili ya kukatalia mipaka sawa sawa hwasikilizani kortini ni kukosea Mwenyezi Mungu.

Pia hawa watoto mnao sikia kwamba wazaliwa nyumbani, ni haki ya yule aliezaa huyu mtoto kijana alinde mtoto wake sio kuniletea mzingo na msichana wangu. Wachukuw mtoto wao na kumlinda.

Pia serikali iwapatie hawa vijana wanao maliza shule na pia college kazi mara moja kuliko kukaa nyumbani na kuandikwa na wazazi tena. Hayo mambo ya makanisa yawe na uhuru wa kuabudu siku ile wanataka wenyewe. Nafikiri sina mengi na Biblia ya zamani ya Kinandi iheshimiwe na pia hiyo Biblia ichapwe. Siku hizi ninaona Biblia imechapwa chapwa lakini ile ya zamani ya Kinandi ile ambayo ilichapwa hiyo kama ingewezekana ichapwe tena. Maanake bii mpya imebadilishwa maneno. Asante sana.

**Com. Riunga Raiji:** Okay asante sana Bwana Samuel, jilandikishe hapo. Moses Cheruoni. Joseph K. Chumo. Vincent Tarusi.

**Vincent Tarusi:** Thank you Commissioners. Mine will be on point form. So the first thing I want the Consitution of Kenya to have a preamble.

There should be a clear separation of powers that is the Executive, Judiciary and Legislature. They should independent of each other. When appoint officials to different position there should be referndum and also qualification should be taken into consideration. There should also be security of tenure. Before increasinn their salaries the MPs there should be also a referendum because nowadays you can see the MPs increasing their salaries any time.

Education, health and poverty should be addressed adequatly by the government.

Security of the people: There is a lot of insecurity in the country at the moment and you find a lot of police road blocks from here up to the Kapsabet you can find five road blocks and yet there is insecurity in the country. So the police instead of stopping vehicles all around they should address the security of the people. Because at the moment Kenya is one among the highest tax country in the world. So I think the tax payment should be made to secure or to give the security of the people since they are paying they should also address education, health and poverty.

Natural resources: Forest should be protected especially finding of indeginous trees.

Land: The Consitution should protect distribution of land by the President e.g IDC land, research land and all state

corporation land and if possible also slum which have been grabbed should be returned before the next Constitution is taken into effect.

General election: General election should be held every five years and they should be fair and free. Electoral offenders should not be pardoned like the Ngei amendment of 1975.

We should also have the Federal type of government where the states are autonomous and there should also be the central government.

Disabled people not be discriminated in the society due to their inability. Also they should be given positions in terms of education, health services etc.

State corporations like cereal boards, KCC, ADC should be protected totally from collapsing by ensuring that the activities are protected from foreign competitors and importation of goods which can be produced locally.

Lastly, county councils should oversee the profits which are from within the area. If they are tea estates, any industries around. The share which are received should be overseen by the county council and then the profits should benefit the people who are within that area. Thank you.

**Com. Riunga Raiji:** Harun Cheryot. Samuel Sambu utafutwa na Christopher Kosgei halafu Peter Rugut.

**Samuel Sambu:** Asante sana Bwana Commissioner. Ka jina naitwa Samuel Kipchuma Sambu kutoka Songoi location. Jambo ambalo mimi nitaliongea ni jambo moja tu. Kuhueu haki ya binadamu na ningependa kuomba Tume hilo jambo liwe katika Katiba ya kurebishwa. Mwananchi wa kenya kukosa ardhi na atukiangalia mbele sana viongozi waliokuwa katika nchi hii wako na zaidi ya elfu hamsini huko na kuna mwananchi mabaya hana ata quarter.

**Com. Riunga Raiji:** Unapendekeza nini?

**Samuel Sambu:** Ninapendekeza apewe haki yake maana ardhi ni ya Mwenyezi Mungu sio ya serikali.

Jambo lingine na la mwisho: kuhusu uchaguzi, kuna neno la kusema uchaguzi ifanywe katika Bunge, kuchagua President achaguliwe na wananchi direct. Ionekane ya kwamba ni kiongozi ambaye anapendwa na watu wote sio Bunge aende achague kiongozi na huko yeye alichaguliwa. Hilo ni la mwisho na sitaendelea. Asante sana

**Com. Riunga Raiji:** Kuna swali mzee.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana Bwana Sambu. Swali langu ni, kuna uhusiano gani kati ya haki za binadamu, na haki za akina mama, na haki za watoto kwa maoni yako?

**Samuel Sambu:** Kuna haki hizi. Hakuma haja mama anyimwe ardhi yake ni ya Mwenyezi Mungu au mwananchi au mtoto. Mambo ya ardhi nimesema ya kwamba ni ya Mwenzi Mungu na kwa nini mtu mmoja awe na acre nyingi na mwananchi yule anateseka na anaitwa mwananchi wa Kenya.

**Com. Riunga Raiji:** Asante umejibu. Christopher Kosgei ambaye atafuatwa na Peter Rugut.

**Christopher Kosgei:** It is in this case I Christopher Kosgei I want to present the following views. Law amendment: Parliament should make by-law until wananchi appeal and be signed by church organization at least 10 to pass as law.

Security: Armed forces make their law and President to stop donation of forces to other nations instead ---- international forces.

Village elders should be given salaries.

Political parties: The ruling party party to be financed by public funds. The losers to be financed by its own members. Other parties to be given Ministries according to ration or force.

System of government: President to remain powerful but not above the law.

Legislature: MP should be a member of the dominated tribe from a given district. No Majors to be given to women only through election but not as local authority. DO and DC should be from the area to present their people.

Executive: The Executive seat to be shared according to votes with the other parties. President should be the head of finalizing decision at the Parliament. Provincial administration should be responsible of law and order of district and church organization to be included in the Executive.

Judiciary: If person violets the law be charged accordingly but the manner of the staying in cell should be abolished. Also the manner of APs caning people as suspect should be stopped and enquire investigation of the victim when he is in cell.

Local government: Mayors and council Charimen be elected directly by the people. They the councils should serve people provided they are elected directly without limitation by empowering them than DC. They should be from with a better grade.

Local authorities seats should be given educated people and those posts at election. Councillors be elected by wananchi and nominated ones be elected also.

Ministry for local government ----- when wananchi have no confidence by abusing his her powers.

Electoral system: simple majority rule as the basis of winning an election. Retaining 25% presentations of Provinces for President. Geographical Constituencies be seen as per previous bounder as for wananchi as when Europeans where in this country.

Death penalty: Death penalties be abolishe instead life sentence.

Land: Only owners who own land are given district but noa anywhere.

Community righthst: Every community's culture should be respected provided it doesn't hurt any other community.

Natural resources: Taxation mostly like county council to be abolished and use only taxation at the already manufactured goods from natural resources. Councillors should protect forest and forest should be property of their area in case of stabalising the community of the area concerned.

International affairs: Parliament to deal with foreign affairs. May I finish?

**Com. Riunga Raiji:** That is the last one. You are finishing that point the rest we shall read the Memorandum

**Christopher Kosgei:** Electoral Commission to be incharge of power during every election but at the grassroot to be DOs. If any form of rigging experience be ----- should be done by different organizations be supervisors. Provision of security and welfare as at power to be administered is not carried normally as the President or any leader. Thank you Sir.

**Com. Riunga Raiji:** Okay, asante Christopher utatupatia hiyo Memorandum. Peter Rugut atafuatwa na Lawrence Sugut.

**Peter Rugut:** Mimi ni Peter Rugut kutoka area hii tu. Neno langu au maoni yangu sio mengi ni yale tu ambayo ninayaona na yale ambayo niliyaona zamani n aya leo.

**Com. Riunga Raiji:** Sema hayo yote.

**Peter Rugut:** Nitasema. Kwa hivyo mimi nitarudi nyuma kidogo, mwaka wa arubani wazungu walikuwa wanatawala kweli katika nchi hii yetu na sheira ambazo hawa walikuwa wanatawala nayo zingine zlikuwa nzuri na zingine baya. Lakini hizo sheria zilikuwa nzuri. Walikuwa wanalinda udongo sana, sana. Walikuwa hawawezi kulima mahali pana mteremko halafu walio salia wakati tulipopata utawala sijui sheria zilirengeshwa namna gani mpaka sasa nchi inaendelea kuwa baya. Kitu kile mimi ninasema ni kwamba iwekwe kwa Katiba hii, milima ambayo watu wanakaa kupandwe miti na mahali forest iko ambapo hakuna kitu kupewe watu sio kwa mlima. Lakini milima yote iwe forest. Hiyo ndio mimi ninaonelea wakati huu. Hakuna maana ya kupiga mikono jamani kwa sababu sisi hatujui kama itawekwa kwa sheria, haya tunasema tu. Kwa sababu kusema namna hii tunafurahia kwa vile awa waliofikiria kutoa Tume ili ipate maoni kwa watu wote wa Kenya. Hii ni mzuri sana kwa sababu kungekuwa maneno mengi yanajulikana. Mimi ninaona hiyo ni nzuri na hilo ni oni langu moja. Forest iwe milimani.

**Com. Riunga Raiji:** Hiyo tumesikia nyingine.

**Peter Rugut:** watu wameisema lakini nitaunga mkono kidogo. Tumsumbuliwa na watoto unajua kuna watoto hawakuelima kwa masomo. Sasa hawa wamezalia nyumbani wanaongezea sisi taabu. Na vile hawa watu wamekwisha sema kuwekwe sheria hii kama mbeleni – irudushwe kwa sababu mwaka wa sitini hii sheria ilikuwa lakini wakati tulipopata utawala ilirudishwa nyuma. Sijui wasichana walifanya nini ndio serikali ikaone hiyo ni biashara ndio ikarudishwa nyuma lakini mimi ninasema irudishwe, kwa sababu wametupa taabu kabisa.

Wazee wapatiwe pesa na serikali, wazee wa kutoka miaka sitini na kuendelea. Kwa sababu sasa ata watoto wetu wanashindwa kutuchunga. Mtoto akileta bibi anakaliwa na bibi yake tunakuwa na taabu wazee. Hayo ndiyo maoni yangu.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana. Lawrence Sugut. Christine Keiyo, karibu.

**Christine Keiyo:** *Ami ng'olyotab in amache koteb Nandiek kou ye ki u.*

**Translator:** Anataka Wanandi wakae vile walikuwa zamani

**Christine Keiyo:** Wakati nilipozaliwa Wanandi walikuwa wanaitwa Wanandi, siku hizi wanaitwa Wakalenjin. Na sisi tunataka Wanandi waitwe, Melegeyo waitwe Waelegeyo, Kipsingis – Kipsingis, vile kuliwa. Mungu alimba namna hiyo jusi jusi tu ndio mimi nilisika Wakalenjin. Sasa mtu anakosa mueleke na kwao, hajui kwao ni wapi.

**Christine Keiyo:** *Kokeny,*

**Translator:** La pili.

**Christine Keiyo:** *kokeny ko kijanaek ak tibik.*

**Translator:** Maneno ya wavulana na wasichana

**Christine Keiyo:** Wakati hule wa rika langu, kulikuwa hakuna msichana anazalia kwao na siku hizi watoto wanakuja

kutumwagia sisi watoto na akimwagia sisi watoto na mimi niko na wangu na yeye anaongeza wake sasa ardhi yangu itakuwa kiasi gani. Maoni yangu mimi ninataka sheria iwekwe sheria kama mtoto akizalia nyumbani achukue mtoto wake apende asipende. *Ngomut lakwennyi chito amun kosiche chito lakwennyi kochome.*

**Translator:** Mtu apeleke mtoto wake kwa vile alizaa akipenda

**Christine Keiyo:** Hakukamatwa kwa nguvu kama angekamatwa kwa nguvu si angeliana watu wangesikia. Kuwekwe sheria tafadhali kila mtu achukue mtoto wake.

*Age kemoche lagokyok arusit keyae, koyai botiriot anan kitun kipgaa.*

**Translator:** Anataka watoto wakioana Pastor ama Padri shikanishe hiyo ndoa.

**Christine Keiyo:** Si DC kwenda kufanyia harusi watoto wetu, na *boiyot tum* yuko nyumbani. *Mi boiyob tum gaa.*

**Translator:** Mze wa sherehe ako nyumbani.

**Christine Keiyo:** *Botiriot ko mi gaa.*

**Translator:** Padri yuko nyumbani

**Christine Keiyo:** *Ngitun lagokyok en gaa kipgaa*

**Translator:** Watoto waoane nyumbani

**ChristineKeiyo:** na hiyo iwekwe kama sheria. *Ang nandiek koyai tumdonyuan kou ye ki u.*

**Translator:** Wandandi wafanye sherehe yao vile ulikuwa tangu zamani

**Christina Keiyo:** *Ara nye koyai tumdonyuan kou ye kiu tumdonyuan si kotok itondonyan.*

**Translator:** Vile sherehe yao ilikuwa -----ionekane vile ilikuwa

**ChristineKeiyo:** *Nga sine kaakemwoe amache kotamwa kora; borosti nebo Nandi korib Nandiek ak koteb komie korib Nandiek borostinnyuan.*

**Translator:** Ingawaje ilikuwa imesemwa forest ya Wanandi ichungwe na Wanandi

**Christine Keiyo:** Iwekwe kama sheria. *Age tugul ne tononi ne moche chochote koik nondindet.*

**Translator:** Mwenye anasimama akitaka chochote lazina awe Mnandi

**Christine Keiyo:** *Mi ng'olyot age yu kora ne atoren.*

**Translator:** Kuna jambo lingine hapa ningependa kumalizia

**ChristineKeiyo:** *Koagas ng'olyot age ne nyone ne u on kibunu chumbek ne kakile kimoche koaechin murenik ak chepyosok.*

**Translator:** Jambo lingine lilitoka kwa wazungu lenye usawa wa wazee na wamama

**Christine Keiyo:** *Ko sheria inata ko makimuchi kiyan. Kimoche koteb Nondindet ak Kwondonyin kou ye ki u.*

**Translator:** Hiyo sheria hatuwezi kukubali. Tunataka Mnandi akae na bibi yake vile ilikuwa tangu zamani.

**Christine Keiyo:** *Amu in kakile inye koek agenge, koaechin murenik ak chepyosok ago kiyae Mungu chepyoso ak muren ak kole wo age.*

**Translator:** ni kwa sababu gani mzee na mama wawe sawa na Mungu ametengeneza wawe tofauti.

**Christine Keiyo:** *Ko kingolen inguno Mungu moche ko wo age ko ng'o age ne kanyokobut ng'atutikab Mungu.*

**Translator:** Mungu alisema mmoja awe mkubwa na mwingine awe mdogo sasa ni nani mwingine avunje hiyo sheria

**Christine Keiyo:** *Kimoche kityo kwoechin kasisiek, kasitab chepyoso ak muren en kasisiek che kisirei, kou Mwalimu, kou nee, kiy age tugul. Tab kebwa gaa konyokotonon ng'atutietab Nondindet kou nikinyeta.*

**Translator:** Tunataka wamama na wazee wawe sawa kwa kazi ya kuandikwa lakini mama akirudi nyumbani mzee anakuwa mkubwa na sheria iwe ile ile kama zamani.

**Christine Keiyo:** *Konyokorib lagok ak boiyot ak kondit nikinyeta bo Nandiek nikinye bo tai*

**Translator:** Wakuje wachuge watoto na ile heshima ya zamani

**Christine Keiyo:** *Lakini kwa kasit kesir sasa amun kikosoman lagokyok ko ingoaechin kasisiek makiyesyoi.*

**Translator:** Wakati wa kuandikwa wawe sawa.

**Christine Keiyo:** *Lakini sheria nebo Nandi kotelel kou ye kiu.*

**Translator:** Sheria ya Wanandi iwe vile ilikuwa.

**Christine Keiyo:** Asante.

**Com. Riunga Raiji:** Asante mama, jilandikishe hapa. Nimeongeza mama muda kwa sababu nimeona hayo mawaidha ametoa ni muhimu zaidi ata kwa wale walikuwa wamesahau mila zao. Bwana David K. Rono. James Kisoriyo, inaonekana hayuko. David Samoel. K.A Cheruiyot utafutwa na Bwana Stephen Tiony

**Kiptarus Arap Cheruiyot:** Jina langu ni Kiptarus Arap Cheruiyot. Maoni yangu ningependelea serikali ya Majimbo, Federal government.

Ya pili, ningependelea mipaka irudushwe vile wazungu walivyo iweka.

The republic of Kenya ni ya nani? Ni ya makabila yote ya Kenya.

Province iwe ni ya makabila yote ambao wanakaa katika hiyo province. Kwa mfano, Rift valley Kipsigis, Nandi, Keiyo, Tugen, Sabaot, Pokot, Masai, Samburu na Turkana wako ndani. Nandi district in ya Wanandi. Public holidays, vile nchi imeharibika kwa uchumi mimi ninaoneolea ya kwamba afadhali watu wafanye kazi kama zamani. Public holidays zipunguzwe. Madaraka day, Moi day, Kenyatta day na Jamhuri day ziwe zote siku moja na iwe Jamhuri day. Na Idi day iwe ya Waisilamu peke yao, watu wengine waendeleo na kazi.

Upande wa kazi: Wafanyi kazi wote wafanye kazi masaa arubaini na sita kwa wiki siku sita. Masaa nane kila siku kutoka Jumatatu mpaka Jumamosi. Na Jumamosi iwe siku ya kufanya kazi dogo dogo, arusi, weekly review, halafu tunarekebisha mambo. Kama sasa nataka kupotea najua kwa ----- mara moja kuliko kukaa kwa muda mrefu. Wafanyi kazi waserikali na parastatals warudishe kuwa hamsini kwa mia, they should be reduced to 50%. Kwa sababu ukienda ofisi unakuta viti ni sita na meza sita lakini wale watu wanakaa ndani ni wawili tu. Hiyo ni kuonyesha ya kwamba wamekuwa zaidi.



**Elimu:** Elimu zamani au juzi michezo yote ya mashule inafaa kufanywa mwisho wa wiki kama Jumamosi. Kumatatu mpaka Jumaa kalamu peke yake. Waalimi vile vile waende wakachukue mshahara Jumamosi. Sio Jumatatu au Jumanne, kile kitu Jumamosi – weekend. Hiyo inatosha. Primary schools serikali itusaidie iwe free education kabisa kabisa. Sio mambo ya kesuma wazazi nunueni vitabu, ooh wazazi fanyeni hii tena, iwe free education from standard one to standard eight fully.

**Parliament:** Mawaziri wanafaa kupuguzwa mpaka kumi na sita hasa wale walikuwa kwa seventy's wabaki kumi na sita, na vile vile mishahara yao irudishwe vile ilikuwa. Ninamaliza sina maneno mengi, mambo ya VAT hayo mambo ya VAT imetumiza sisi wakulima kabisa. Na jambo hili la VAT liondolewe kabisa kabisa na zaidi kwa upande wa ukulima, kila kitu, -----, fertilizers lets say all the imports VAT should be scrapped completely. Asante sana Bwana Chairman.

**Com. Riunga Raiji:** Njoja kidogo niko na swali kwa sababu tuko karibu kumaliza na tumesikia hili jambo la mipaka irudishwe vile ilikuwa zamani lakini labda ningetaka unieleze kwa sababu wewe ni mzee ni shida gani iko kwa mipaka ya Nandi district.

**Kiptarus Cheruiyot:** Mimi sio mzee sana, mimi bado ni kijana. Hii mipaka tangu wakati wa ukoloni tuliishi vizuri sana bila vita yoyote. Akukuwa na clashes, clashes kuna kitu kinafichwa ndani yake ingewekwa land clashes ndio ingeonekana vizuri. Tangu wakati wa uhuru watu wamehama hama kufika pale tabia za watu wengine na wengine hazifanani, sasa ndiyo zinaleta mambo ya clashes. Kama mipaka ingekuwa vile ilikuweco zamani, mimi nikuja kukochokosa wewe huko serikali inaangalia kwa nini mimi ninaruka hapa nakwenda kuchokoza hule. Kama wewe unakuja kunichoza mimi hapa serikali inaangalia lakini siku hizi mipaka inasongeshwa, inasongeshwa pole pole, pole pole na hivyo si vizuri. Watu wakae vile walikuwa wanakaa. Asante sana.

**Com. Riunga Raiji:** Okay nafikiri tuko na sqwali lingine kutoka kwa Commissioner.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana Bwana Cheruiyot, umesema kuwa mambo mengi tuyaleta mwishoni mwa wiki kwa siku ya Jumamosi na hasa mambo ya shule. Kuna watu wenye kuabudu siku ya Jumamosi wanaitwa Seventh day Adventist, kila pahali penye tumeenda isipokuwa hapa wamekuja kupendekeza kuwa Jumamosi iwe siku ya Sabato. Na shida zao nyingi zimekuwa kwa wanafunzi wao wanapoenda shule zenye zinaleta mambo nyingi mpaka saa zingine michezo na kila kitu siku hiyo ya Sabato. Wewe mzee kijana umeona mengi, ungetueleza aje juu hii vile tunataka kufanya kazi na pia tunataka keheshimu hizi dini tofauti.

**Kiptarus Cheruiyot:** Asante sana Madam, ata hapa kuna Seventh Day labda ujasikia kunayo. Na wanabudu Jumamosi hiyo ni kweli lakini nilikuwa nasema mambo ya sports peke yake. Kwa sababu unaweza kuona haya mambo ya michezo ya mashule kutoka Jumatatu mpaka Jumaa, hakuna shule. Michezo kesho, michezo kesho, mishezo kesho, wanaenda locational, wanaenda divisional, wanaenda distrit, mpaka wiki inakwisha bure. Lakini hao wanaweza kuenda kanisa sijakataza mtu, huwezi kukataza mtu kanisa yake. Laikini hapa sisi tuko na Seventh day kweli kweli.

**Com. Riunga Raiji:** Okay asante sana sitakuita mzee au kijana, Bwana Cheruiyot.

**Kiptarus Cheruiyot:** Mzee sio baya. Unajua ukisema mzee ni yule mtu amekwisha kwenda zaidi na mimi mtu wa juzi juzi. Nafikiri haya yametosha. Asante sana.

**Com. Riunga Raiji:** Jiandikishe. Nilisema sasa - Stephen Tiony.

**Stephen Tiony:** Kwa majina ni Stephen Tiony. Sitakuwa na mengi ya kuongea kwa vile nikiongea mengi nitakuwa nikirudia yale watu wameongea. Kitu ambacho ningetaka kuguzia ni wakulima. Mkulima sana sana uwa ananyanyaswa, ukiona kama cess inapelekwa Nairobi halafu inarudushwa tena ikuje ifanywe kazi hapa, kwa nini cess ikatwe hapa nyumbani halafu ile inapelekwa ipelekwe Nairobi, badala ya kupelekwa huko halafu iridishwe tena. Ninaona heri cess ikatwe nyumbani halafu ile inabaki inaenda juu halafu ingawanywa kado kado kuanzia hapo.

Viongozi wetu hawajui kazi yao. MP is not a must for him to a Minister. Minister ni mtu mwengine tofauti kazi yake ni tofauti na ya MP. Ningeonelea ya kwamba Constituency kama hii yetu, tungekuwa na Minister mmoja, hata na Wabunge wawili au watatu halafu kazi iendeleo haraka. sasa tunakuwa na Minister mmoja na yeye ni Mbunge na PC, nchi hii yetu kubwa, halafu sisi tunakosa namna, maendeleo inaenda pole pole zaidi.

President sio lazima awe na kazi ingine kana Minister ama nini, mtu mmoja ambaye anapaswa kuwa Mbunge ni mtu kama Vice President. Mimi ninaona kazi ya Vice President sio kazi kubwa anapaswa kupewa kazi kama Mbunge au Minister. Lakini President kazi yake ni kubwa na anapaswa kutengemea hiyo moja. Kwa maana mtu mmoja alizaliwa na tumbo moja kwa nini uwe na kazi nyingi na unakula na tumbo moja. Inapaswa uwe na kazi moja halafu mwezako awe kazi hiyo ingine. One man onejob halafu kazi iende haraka. Mimi ninaona ingekuwa namna hiyo. Sian mengi ya kuongea.

**Com. Riunga Raiji:** Okay, asante sana. Stephen jiandikishe. Sasa kulingana na list ya wale watu walikuwa wamejiandikisha na kuandika kwamba walikuwa wakitoka kutoa moani inaoonekana tumemaliza, wa mwisho alikuwa ni Stephene. Sasa sijui labda kama kuna mtu alirukwa na angetaka kutoa maoni. Kama kuna yeye tafadhali anue mkono tumuone. Yule ambaye hajaongea. (Interjection inaudible) hapana nimesema yule hajapata nafasi ya kuongea sio yule anataka kuongeza. (Interjection) hio utanibia tukitoka. Na nyinyi mlijiandikisha? Na mlikuwa mmependekeza kuwa mnataka kuzungumza ? Semeni ukweli kwa sababu tuko na list hapa. Wewe ukijandikisha, na wewe Bwana?

**Speaker:** Nilijiandikisha kama observer.

**Com. Riunga Raiji:** kama ulikuwa observer. Okay umenguzia nia, hata hiyo sio baya. Na wewe Bwana? Ulikuwa observer, ata hiyo sio baya. Sasa nyinyi watatu mtamalizia. Kila mtu dakika mbili mbili ili sasa tuweze kumaliza kikao. Wewe ndiwe tutaanza nawe, sema jina na utatuambie tu ile ya muhimu utatupatia Memorandum. Dakika ni mbili.

Elijah Vitengede: Okay, thank you very much Commissioners. My names are Elijah Vitengede. I am going to talk about a few thinkgs which I have felt that there are really touching very much on our Constitutional Review. We should look on the side of religion: we should have limitation on the side of freedom of worship and this will curb things like devil worship which has actually affected various institutions in this country.

Education: it should be made compulsory and free in all the nurseries and primary schools. We should make sure or is my suggestion that we should have a contant and stable syllabus instead of having syllabus being changed from time to time.

Corporal punishment: it should be reintroduced but with limitations this will curb compulsory in all schools however other subjects should also be considered which should be compulsory. For example computers.

We should have separation of power in all the three organs of the government that is the Judiciary, Legislature and the Executive. This will make sure that there checks and balances. Thank you very much.

**Com. Riunga Raiji:** Asante for being precise and to the point and being within you two minutes. Na wewe Bwana sema jina lako.

**Wilson Cheruiyot:** Kwa majina mimi ni Wilson Cheruiyot. Niko na mambo mawili tu peke yake. Kwanza ningependa kuongea kuhusu hili jina la State House. Kama vile jina linatambia State House nafikiri ni nyumba la republic of Kenya. Lakini jambo la kushangaza ni kwamba mtu kama mimi wakati unapofika wakati wa kura ninaitajika kupigia kura Rais. Lakini kufika State House ni taabu, kwa hivyo ningependekeza State House iwe free, kila mtu awe na nafasi ya kuenda kuona Rais kwa sababu anahitaji kura yake.

Pili, ningependa yale mambo ya cost sharing. Yenyewe ni safi lakini ningependa ifanyiwe marekebisho kidogo tu pahali pachache – upande wa hospitali. Kwa sababu ugonjwa sio kitu mtu anaweza kupanga au mtu uwa hajui ni siku gani atakuwa mgonjwa ingefaa kuwe na mpango fulani ambao watu watatibiwa bila maneno ya cost sharing. Iwe free ata kama ingewezekana card fulani ingetolewa kwa wananchi wa Kenya ili kila mtu alipe kila mwaka. Hiyo itasaidia kwa upande wa matibabu. Yangu ni hayo tu.

**Com. Riunga Raiji:** Asante sana, jilandikishe na wewe kijana. Sorry I have misdiscribed you ni mzee. Lakini tuliambiwa tusiite watu wazee sana.

**Geoffrey Kipsang Moi:** Thank you Commissioners. First I am Geoffrey Kipsang Moi. My first issue id pertaining Presidential powers. I think the Constitution should reduce the powers of the President. The President should not be above

the law but should be someone who should adhere to the Constitution. And I remember there was a case where our Excellency had to keep us in suspense for sometime before he reappointed the Vice President. I think such case should not arise or should not be repeated.

Lastly, I am proposing that in the new Constitution the idea of using tribal names for districts should be abolished and a case in point is Nandi district. In Nandi district there are other communities which are living in Nandi but these non-communities feel sort of discriminated because the Nandi's are claiming we are in our land. What about those who are not Nandi's? I can give you an example some of us who are living at the margin of Nandi district at times we do say we are going to Nandi so I don't know where this Nandi is. Yet I am living in Nandi district. So these districts which were named after tribal names like Keiyo, Nandi etc I think in the new Constitution we should try to coin other names which can be used to suit all the people who are living in those districts,. Otherwise thank you.

**Com. Riunga Raiji:** Just one clarification. You said something about the Vice President but I didn't get. What was your proposal. You said we were left without a Vice President for sometime.

**Geoffrey Kipsang:** I said the President should be somebody who adheres to the Constitution. I think the Constitution provides for the President to appoint the Vice President. And I don't see the reason why a President can keep us for a ride for sometime and then he reappoints the same person.

**Com. Riunga Raiji:** I got your point you have basically recommended that the President must adhere to the Constitution because the Constitution provides for the appointment of a Vice President. I think you have made your point very well. Thank you very much Geoffrey Kipsang Moi and we that sasa tumefika mwisho wa kikao cha leo cha Tume ya Kurekebisha Katiba. Na tungetaka kwa niaba ya Chairman wa Commission, Makamishena's wezangu Salome Wairimu Muigai huyu na Domiziana N'tochekera Ratanya, na mimi Riunga Raiji tungetaka kuwashukuru sana kwa vile mlikuja kwa wingi. Tumekaa pamoja na mmetoa mapendekezo mkiwa huru kabisa na sisi tume-record yote na ingine tumeandika na tungetaka kuwakikishia kwamba tuyatumia wakati wa kurekebisha Katiba. Tungetaka hasa kuwashukuru sana Mrs. Kosgei na team ya Members of the Constituency Committee, halafu Father Kigen, Bwana Tororey Mkuu wa hapa ambaye amekaa nasi tangu asubuhi na ata kuruhusu watoto waje wasikilize na wachagie mambo ya Kikatiba.

Nafikiri kabla hatujamliza Martin Cheruiyot atufungie kwa maombi, ningetaka kumliza coordinator wetu ambaye ni mama hapa Mrs. Kosgei labda aseme neno moja au mbili halafu tutafungiwa na maombi.

**Mrs. Kosgei:** Kwa Commissioners ambao wamekuja Nandi, Bwana Ratanya, Chairman Bwana Riunga na Salome. Nimesema asante sana na pia watu wanaosaidiana pamoja kwa kazi yenu jema ambayo mmefanya kwa amani, nimefurahia, wananchi wamefurahia. Nashukuru pia wananchi kwa maana mmkuja kwa wingi. Asante sana Head master wa shule na Father

